SINCE 1922

# eabl

CELEBRATING LIFE




# 2022 INTEGRATED REPORT & FINANCIAL STATEMENTS

# Taarifa ya Meneja Mkurugenzi na CEO wa Kundi

## Kujenga msingi wa ukuaji kwa ajili ya miaka 100 ijayo

Nina furaha kwamba tumeandikisha mwaka mwingine wa matokeo mazuri na thabiti ya kifedha katika East African Breweries PLC (EABL). Katika mwaka wa kifedha wa 22, kampuni yetu ilipiga hatua katika kutimiza lengo lake la kuwa moja ya kampuni ya kutengeneza bidhaa iliyo bora zaidi, inayoaminika na kuheshimika zaidi. Mwaka huu wa 2022 EABL inasherehekea miaka 100 tangu kuanzishwa kwake na ningependa kuwashukuru wafanyakazi wetu wote kwa kuendelea kuwa wakakamavu na wenye kujitolea.

Katika nusu ya kwanza ya mwaka huo wa kifedha, tulishuhudia kuondolewa kwa vikwazo na masharti yaliyokuwa yamewekwa kutokana na janga la COVID-19 kote Afrika Mashariki na hili lilichangia kufunguliwa tena kwa uchumi na pia baa na maeneo mengine ya kuuzia bidhaa zetu kwa wateja. Kkutokana na hili, shughuli za kibiashara zilirejelea hali ya kawaida. Wateja walivyokuwa wanarejea kwenye biashara, tulisaidia kufunguliwa tena kwa baa, ambapo tuliwekeza zaidi ya $5 milioni katika kipindi hicho cha janga kusaidia kufufua vituo vya kuuzia bidhaa zetu.

Wakat iwa janga, tulishuhudia mabadiliko makubwa miongoni mwa wateja wetu na wanaotumia bidhaa zetu pia. Kwa kutumia data na habari za kina, tuliwekeza kwa njia ifaayo ili kufahamu mabadiliko hayo na pia tukafanyia uvumbuzi na maboresho bidhaa zetu kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya watumiaji wa bidhaa yaliyokuwa yanaibuka. Kadhalika, tulifanyia uvumbuzi njia mpya za kumfikia mteja na kuwekeza katika biashara ya dijitali na pia kuboresha mfumo wa hatua ya mwisho ya kufikisha bidhaa ili kuhakikisha bidhaa zetu zinapatikana kwa njia rahisi.

Mambo haya yalituwezesha kuandikisha matokeo bora zaidi katika miaka ya hivi karibuni ukiangalia vigezo vyote, na hili ni jambo la kujivunia kwa kila mtu anayehusishwa na kampuni hii kuu.



### Matokeo

Licha ya hali ya changamoto, tuliandikisha matokeo mazuri Mwaka wa kifedha wa 22, ambapo mauzo halisi ya EABL yalikua kwa 27% hadi Kshs 109.4 bilioni. Kulikuwa na ukuaji wa zaidi ya asilimia kumi katika masoko yetu yote. Tuliandikisha pia matokeo mazuri katika sehemu kuu za mikakati: bia ilikua kwa 27%, vileo vikali kwa 27%, vileo vya ubora wa juu kwa 26% na vileo vipya kwa 35%.

Tulifanikisha matokeo haya kwa sababu ya kuendelea kuangazia mkakati wetu na pia utekelezaji wake. Kadhalika, kwa kuwa na mkusanyiko wa bidhaa imara na zinazopendwa.

### Kuunda thamani

Mazingira yetu ya kuendesha biashara yanaendelea kuwa ya kutotabirika hata zaidi, na kuna changamoto kubwa kuhusiana na mitindo ya mabadiliko ya kiuchumi katika kazi ya kanda na hata kimataifa na pia kwenye mazingira ya kiuchumi yenyewe.

> **EABL inabadilika na kuwa kampuni inayokumbatia zaidi ukuaji wa biashara na ubunifu. Matokeo yetu mazuri ya kifedha yalitokana na kuangazia watumiaji wa bidhaa, kasi katika utekelezaji na wepesi wa wafanyakazi wetu kubadilika kuendana na mabadiliko katika mazingira.**

Isitoshe, bado kuna hali ya wasiwasi kuhusu mabadiliko katika kodi na sera katika serikali katika mataifa ya kanda hii.

Biashara yetu haijakingwa dhidi ya misukosuko hii lakini kina na upana wa bidhaa zetu pamoja na nidhamu yetu na kuangazia wafanyakazi wetu vitatusaidia kupitia misukosuko hiyo. Tunapoadhimisha karne moja ya uwepo wetu, EABL imejitolea kujenga kampuni itakayonawiri zaidi ya miaka 100 ijayo.

Mkakati wetu ni kuendelea kuzalisha bidhaa za kiwango cha hali ya juu, uendelevu katika kupanua biashara na kuongeza faida sambamba na uwekezaji katika nembo zetu na biashara. Tutaendelea kuwaangazia wateja wetu na watumiaji wa bidhaa zetu, ukuaji endelevu, uwekezaji wa busara, mkakati wa Mazingira, Jamii na Utawala na pia watu wetu.

## Watu na utamaduni wetu

EABL inabadilika na kuwa kampuni inayokumbatia zaidi ukuaji wa biashara na ubunifu. Matokeo yetu mazuri ya kifedha yalitokana na kuangazia watumiaji wa bidhaa, kasi katika utekelezaji na wepesi wa wafanyakazi wetu kubadilika kuendana na mabadiliko katika mazingira.

Tunakuza kwa kasi utamaduni wa nidhamu na kufanya mambo kwa njia bora zaidi. Hili limechangia kuokolewa kwa fedha nyingi ambazo zimewekezwa tena katika maeneo ambayo tuna fursa bora zaidi. Uwekezaji huu sio tu kwamba unasaidia ukuaji wa bidhaa na nembo zetu na kuimarisha mseto wa bidhaa zetu bali pia umetuwezesha kuboresha uwezo wetu wa kufanya mambo kupitia teknolojia mpya na utoaji wa mafunzo.

Moja ya sifa kuu za EABL katika karne moja iliyopita imekuwa ni usaidizi na uungaji mkono wa wafanyakazi wetu. Tumejenga muundo wa usimamizi unaohakikisha huwa tunaajiri watu bora zaidi kutoka kwa taasisi za elimu na kisha kuwapa mafunzo na kuwapa mazingira bora zaidi ya kunawiri.

## Uendelevu

Kama biashara ambayo imekuwepo kwa miaka 100, tunajivunia kuwa tuna baadhi ya nembo za bidhaa maarufu zaidi duniani. Hizi ziliundwa na vizazi vya watu walioelewa umuhimu wa kuunda biashara na kuiweka sawa kwa ajili ya kipindi kirefu. Tumejitolea pia kuunda biashara itakayokuwa na matokeo ya kufaa katika masuala muhimu kwetu na kwa jamii kwa jumla.

Kujitolea kwa EABL katika uendelevu ni kiungo muhimu sana kwa biashara yetu kuhakikisha inadumu zaidi ya karne ijayo. Juhudi zetu kwa mazingira, ujumuishaji wa wote, uthamini wa watu wa asili mbalimbali na kuendeleza unywaji pombe wa kuwajibika kupitia mpango wetu wa miaka 10 wa ESG ni nguzo muhimu sana katika mkakati wetu wa kuhakikisha tupo katika nafasi nzuri kibiashara na pia kuwavutia watu wenye vipaji.

Tumeshirikiana na wadau muhimu katika sekta ya kibinafsi, serikali, na mashirika yasiyo ya kutengeneza faida, ili kutekeleza mipango yetu ya uendelevu kwa mapana. Mpango wetu wa Wrong Side of the Road (Upande Usiofaa wa Barabara), unaohamasisha mabadiliko ya mtazamo kuhusu kuendesha gari ukiwa umelewa, umewafikia watu zaidi ya 30,000 Afrika Mashariki.

Katika mwaka wa kifedha wa 22, SMASHED, mpango wetu unaoangazia kukabiliana na unywaji pombe miongoni mwa watu wasiotimiza umri ulioruhusiwa, umewaelimisha watu zaidi ya 48,000, au 137% zaidi ya tulivyotarajia. Tulitumia pia DRINKiQ, kifaa chetu cha kuhamasisha unywaji pombe wa kuwajibika, kuwafikia zaidi ya watu 104,000 kuhusu unywaji pombe wa kuwajibika – 317% zaidi ya lengo letu.

> **Tumeendelea kuimarisha mkakati tulioutayarisha katika miaka miwili iliyopita, unaohitaji wepesi wa kubadilika pamoja na kuangazia mahitaji ya wateja wetu kila wakati huku tukijizatiti kutoa thamani kwa bei stahiki kwa kila mteja.Tumeendelea kuimarisha mkakati tulioutayarisha katika miaka miwili iliyopita, unaohitaji wepesi wa kubadilika pamoja na kuangazia mahitaji ya wateja wetu kila wakati huku tukijizatiti kutoa thamani kwa bei stahiki kwa kila mteja.**

Katika safari yetu ya kuwajumuisha watu wa sifa na asili mbalimbali, tuna furaha kwamba tumeendelea kupiga hatua katika kujenga kampuni inayojumuisha wote na kuthamini watu wa asili mbalimbali: 36% ya viongozi wetu wa ngazi ya juu na 63% ya wanaonufaika na miradi yetu ni wanawake, mtawalia.

Kadhalika, tumepiga hatua mwaka huo katika kutekeleza malengo yetu ya uendelevu ya mpango wa kuanzia kwa nafaka hadi kwa gilasi, tukiangazia zaidi uhifadhi wa maji, kuongeza kasi juhudi za kupunguza uzalishaji wa gesi ya mkaa na kwa jumla kuwa biashara yenye uendelevu. ***(Endelea kusoma ukurasa 68-75)***

## Tukisonga mbele

Tunapoingia katika miaka 100 ijayo tukiwa na sifa na msingi tulioujenga, tunaendelea kujitolea kukuza biashara yetu kwa njia endelevu, tunapoendelea kuhakikisha tunatoa thamani ya kipindi kirefu kwa wadau wetu.

Ingawa mazingira ya nje yamesalia kutoweza kutabirika, tunaendelea kuangazia macho yetu katika kutekeleza mambo makuu kwenye mkakati wetu. Watumiaji wa bidhaa zetu wanasalia kuwa muhimu sana kwa biashara yetu na tutaendelea kuwekeza katika nembo zetu za bidhaa na kutumia vyema mseto wetu wa bidhaa kuongeza thamani ya biashara yetu sokoni na kukuza faida. Tumeboresha uendeshaji wa shughuli zetu kote katika baishara yetu kupitia mikakati yetu ya kuimarisha uzalishaji. Hili litahakikisha ukuaji wetu unaendelea, kuboresha wepesi wetu wa kubadilisha mambo inapohitajika, na kuhakikisha kuna mzunguko wa pesa kwenye kampuni yetu.

Tuna imani kwamba tukifanya haya, pamoja na sifa za kipekee na vipaji vya wafanyakazi wetu, tumo katika nagasi nzuri ya kupitia changamoto na kutumia vyema fursa zitakazojitokeza na hivyo basi kuendelea kuchochea ukuaji endelevu wa biashara yetu kote Afrika Mashariki, kukuza nembo zetu za bidhaa na kusaidia masoko yetu kusherehekea maisha, popote.

**Bi. Jane Karuku**
**Meneja Mkurugenzi wa Kundi & CEO**